

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA

SHULE YA SEKONDARI KISANGARA

S.L.P 346 MWANGA, PHONE 0757-800967/0673-199763/0757-784834

15.12.2020

Kumb. Na KSS/F1/KS/2021

FORM Na.....

KWA.....

S.L.P.....

.....

YAH: MAELEZO/MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA WA MASOMO 2021

UTANGULIZI.

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa mwaka wa masomo 2021 katika shule ya sekondari kisangara. Kwa niaba ya Bodii ya shule na jumuiya ya kisangara sekondari tunakupongeza sana kwa kuchaguliwa kwako kujiunga na shule hii. Shule itafunguliwa siku ya jumatatu tarehe **11.01.2021 saa 1:00** asubuhi. Tafadhalii fika na mzazi / mlezi tarehe hiyo kwaajili ya mkutano wa wazazi na makabidhiano.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

Sare za Shule

a) Sare za shule hii ni suruali (mbili) kwa wavulana na sketi mbili kwa wasichana

b) Hijabu zenyne mapambo na urembo hazitakiwi shulenii

Shule inasisitiza kuwa ni vyema kufuata maelekezo yatolewayo mara kwa mara kuhusu sare za wanafunzi ili kuthibiti sare zisizokidhi vigezo na maadili ya kitanzania kwa mwaka huu.

Sare za shule, Mzazi / Mlezi utamshonea mwanao mwenyewe ila ni vyema sare hizo zikashonewe kwa fundi **FARAJI MNDEME** wa kisangara mwenye namba **0754530170** ili kuepuka mchanganyiko wa rangi na ubora wa kitambaa wa sare hizo. Sare ambazo zitakaguliwa siku ya kuripoti shulenii ni kama ifuatavyo:

1. Mashati mawili meupe mapya yenyne mikono mifupi yatakaguliwa siku ya kufungua shule
2. Viatu vya ngozi jozi mbili (02) Rangi nyeusi visivyo na visigino virefu vyenye kufunga na Kamba

3. Soksi jozi mbili nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana
4. Suruali mbili kwa wavulana ziwe na rinda mbili kila upande na pindo la nje (02)
5. Sketi mbili kwa wasichana mshono wa aina ya rinda box yenye urefu wa inchi saba (7) kuanzia magotini kushuka chini. (kitambaa kimeambatanishwa)

NB:Ni mwiko kwa mwanafunzi wa shule hii kuva sketi fupi kwa wasichana au mlegezo na kubana (modo) kwa wavulana hivyo hakikisha unashona sare kulingana na maelekezo ya hapo juu.

6. Sweta maalumu kwaajili ya baridi utapatiwa sampo shulen i umnunulie mwanao pamoja na Tshirt za shule ni lazima kwa kila mwanafunzi.
7. Mkanda mweusi wa ngozi kwa wavulana

Mahitaji mengine

- 1) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli na kijiko)
- 2) Fagio za chelewa kwaajili ya kufanya usafi wa mazingira
- 3) Jembe (wavulana)
- 4) Slesha (wasichana)
- 5) Ndoo ya lita kumi 10 (wavulana na wasichana)
- 6) Mopa (wasichana)

Mahitaji binafsi

1. Madaftari makubwa (counter book)-10
2. Daftari ndogo -9 kwa ajili ya mazoezi
3. Mkebe (mathematics set)
4. Begi la shule kwa ajili ya kubebia madaftari
5. Vitabu binafsi vya masomo kulingana na uwezo wako
6. Kamusi ya kiingereza (English dictionary) ni lazima
7. Penseli na kalamu za kutosha pamoja na rula

NB: dictionary ya English kwa English ni lazima kila mwanafunzi anaripoti kwa mara ya kwanza kwa kidato cha kwanza aje nayo itakaguliwa siku ya kuripoti shule.

Nidhamu kwa ujumla

Ni vyema kukumbuka kuwa jukumu kuu utakalo kuwa nalo katika kipindi chote uwapo kisangara sekondari ni taaluma hivyo ni lazima kwa mwanafunzi kuheshimu na kufuata sheria na taaratibu zote za shule ambazo utapatiwa mara tu ujapo shulen ili kuepusha kuwa na makosa ya kinidhamu hivyo mwanafunzi ni lazima awe mtii, mwaminifu, mfanyakazi hodari,mwenye ushirikiano na wenzake na mwenye kujibidiisha katika masomo yake.

Sare za michezo

1. Raba za michezo
2. Jezi ya rangi ya blue

Chakula cha mchana

Miongoni mwa majukumu ya mzazi/mlezi pamoja na bodi ya shule ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata chakula cha mchana shulenii. Hivyo siku ya kikao cha kufungua shule wazazi/walezi mtakutana na kamati ya wazazi kujadili gharama za chakula hicho cha mchana kwa wanafunzi wenu.

Taaluma.

Kutokana na uhaba wa waalimu wa sayansi,wazazi katika kikao hicho pia mtajadiliana ni namna gani mnaweza kupata mwalimu wa muda au wakujitolea angalau kupunguza uhaba huo.

Pamoja na maelekezo yote hapo juu hakikisha unakuja shulenii na taarifa zifuatazo:

- a) Taarifa ya upimaji wa afya yako kutoka katika hospitali ya serikali **fomu “A” imeambatanishwa**
- b) Fomu ya kukubali kufuata sheria na taratibu za shule **fomu “B” imeambatanishwa**.
- c) Fomu ya taarifa binafsi za mwanafunzi **fomu “C” imeambatanishwa**.
- d) **Fomu “D”** inaonyesha baadhi ya makossa na adhabu zinazowenza kuchukuliwa (Tafadhalii soma kwa umakini)

Mwisho

Mzazi au mlezi hakikisha unakamilisha maagizo yote hapo juu ili kuepusha usumbufu wakati wa usajili. Kwa niaba ya bodi ya shule na wanajumuiya ya kisangara sekondari napenda kukukaribisha katika shule yetu kwa pamoja tuijenge shule yetu.

KARIBU SANA

AHSANTE

.....

ALFRED.M.MOSHA

MKUU WA SHULE